

**OFISI YA RAIS,  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO**



Telephone: 0262968010  
Fax: 0262968010  
Website: [www.kilolodc.go.tz](http://www.kilolodc.go.tz)  
Email: [ded@kilolodc.go.tz](mailto:ded@kilolodc.go.tz)/[ded.kilolo@iringa.go.tz](mailto:ded.kilolo@iringa.go.tz)

S.L.P2324,  
KILOLO .  
Tanzania .



Kumb. Na. KDC/A.3/20/VOL.II/64

23/07/2021

**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI**

Kwa mujibu wa kibali cha Ajira Mbadala chenye Kumb Na: FA/170/363/01 "A"/46 cha tarehe 04/05/2021 cha kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa ya kutuma maombi ya nafasi ya kazi ya Mtendaji wa Kijiji Daraja la III kwa kuzingatia vigezo na masharti yaliyopo katika tangazo hili.

**1. MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA LA III (VILLAGE EXECUTIVE III) - NAFASI 2:**

**a) SIFA**

- Awe amehitimu Elimu ya kidato cha IV au VI na awe amehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti cha Technician Certificate (NTA level 5) katika moja ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka katika Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo - Dodoma au Chuo chochote kinachotambulika na Serikali.

**b) KAZI ZA KUFANYA/MAJUKUMU**

- Atakuwa Mtendaji na mshauri wa Serikali ya Kijiji na Kamati zake katika mipango ya maendeleo.
- Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji na atasimamia mapato na matumizi ya Halmashauri ya Kijiji.
- Atakuwa mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji.
- Atapaswa kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango na Maendeleo ya Kijiji.
- Atatafsiri Sera, Taratibu na kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo za Halmashauri ya Kijiji.
- Atakuwa Katibu wa Kamati ya Halmashauri ya Kijiji.
- Ataongoza vikao vya maendeleo ya kijiji vitakavyowahusisha wananchi na wataalam waliopo kwenye eneo lake.
- Atapaswa kuhamasisha wananchi katika mikakati mbalimbali ya kuondoa njaa na umasikini.
- Atakuwa kiongozi wa wakuu waldara na vitengo wa kitaalam katika kijiji

c) **NGAZI YA MSHAHARA**

- Mshahara ni kwa mujibu wa viwango vya mishahara Serikalini yaani TGS B<sub>1</sub> = (TSHS.390,000/=) kwa mwezi.

d) **Masharti kwa ujumla:**

- Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenyewe umri kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- Waombaji waambatanishe Cheti cha kuzaliwa
- Waombaji waambatanishe maelezo binafsi (CV) yenye anwani na namba za simu zinazopatikana pamoja na majina ya wadhamini watatu (Referees) wa kuaminika.
- Maombi yote yaambatane na vyeti vya Elimu na Taaluma yaani nakala za vyeti vya kidato cha nne au sita, pamoja na vyeti vya Taaluma (Professional Certificate from respective board, Computer certificate) na picha 2 (passport size) za rangi za hivi karibuni.
- 'Testimonials' Provisional Result, Statement of Result, hati ya matokeo ya kidato cha Nne na kidato cha sita **havitakubalika kabisa**.
- Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (NECTA NA NACTE) na taarifa ya ulinganifu iambatanishwe kwenye maombi.
- Waombaji wa nafasi za ajira waliostaafishwa, waliofukuzwa kazi na kuachishwa kazi katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Ras, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.
- Barua ya maombi iandikwe kwa **mkono na kwa lugha ya Kiswahili** tofauti na hapo ombi lako halitapokelewa.
- Barua ya maombi isainiwe na mwombaji mwenyewe tofauti na hivyo maombi hayo yatakataliwa.
- Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- Waombaji watakaokidhi sifa na vigezo watajulishwa tarehe ya usaili kwa namba za simu na anuani walizotumia kwenye barua ya maombi
- Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni **tarehe 06/08/2021 saa 9:30 Alasiri**.
- Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta kuititia anwani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji (W)

Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo,

S.L.P 2324

**KILOLO.**

Imetolewa na:

Lain Kamendu

Mkurugenzi Mtendaji (W)

KILOLO

*[Signature]*  
MKURUGENZI MTENDAJI WA WILAYA  
KILOLO

**NB:** Tangazo hili linapatokana kwenye mbao zote za matangazo za Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo na kwenye tovuti (website) ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo ambao ni [www.kilolodc.go.tz](http://www.kilolodc.go.tz)